

# MUHOGO

Ni zao muhimu la chakula na katika kutekeleza sera ya Taifa ya kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi zinazotokana na sekta ya kilimo.



- Tanzania ni nchi ya **6 barani Afrika kwa uzalishaji wa zao la muhogo na ya 11 duniani**
- Zao hili ni la muhimu na la kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDPII) katika Kanda za Pwani, Ziwa na Kusini.

## KILA SEHEMU

### YA ZAO HILI INA MATUMIZI

**Majani, shina na mizizi**

#### Una Protini na Vitaminini

kwa wingi



Hutumika  
kama kipando

Una kiasi kikubwa cha wanga kinachotoa kalori zinazohitajika kwa wingi katika mwili wa mwananadamu **na ni bidhaa muhimu ya viwandani.**

Fursa zipatikanazo katika zao la muhogo - kama zao la chakula nala biashara



Mhogo  
unastahimili  
ukame

Chanzo muhimu  
cha chakula na  
kipato

Zao la  
maendeleo ya  
viwanda vijijini  
vinavyotegemea  
kilimo kupitia  
shughuli za  
usindikaji

Ni mojawapo wa  
**vitu muhimu  
vinavyotumika**  
kuandaa chakula  
cha wanyama na  
kutengeneza  
**bidhaa za  
chakula zenye  
ubora kama vile  
biskuti, keki,  
mikate na  
maandazi**

Unatoa **fursa ya  
kupunguza  
matumizi ya  
fedha** za kigeni  
zinazotumika  
kuagiza malighafi  
za kutengeneza  
bidhaa za  
viwandani kama  
**vile wanga,  
viungo vya  
kuongeza ladha  
kwenye vyakula,  
pombe gundi  
vidonge pamoja  
na 'ethanol'**

## FURSA ZA KIPATO

### Kuungeza uzalisha wenye tija

- Kuungeza uzalishaji kutoka tani 6 kwa Hekari Moja hadi Tani 30 kwa hekari mojaka kutumia teknolojia za kisasa mfano matumizi bora ya mbolea, aina ya pembejeo zilizoboresha, na uzalishaji i wa haraka wa mbegu za muhogo - Semi-Autotrophic Hydroponics (SAH).
- Zaidi ya aina 20 ya mbegu bora za muhogo iliyoboresha zimesambazwa na zipo katika taasisi za utafiti
- kuhamasisha matumizi ya mashine na zana bora katika uzalishaji wa zao la muhogo.




### Kuungeza ufanisi na fursa za masoko katika sekta ya usindikaji




- Kuhamasisha matumizi ya teknolojia na mashine za kisasa za usindikaji
- Kuhimiza matumizi ya yakanuni za taratibu zitakazosaidia kufikia ubora na viwango vya kimataifa

### Kuungeza fursa za masoko kwa wazalishaji



### Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi



- Kutoa msaada wa kiufundi katika kuendeleza viwanda vya usindikaji wa mazao katika maeneo ya vijijini
- Kuungeza fursa za upatikanaji wa mikopo

*Kusafirisha nje ya nchi bidhaa za muhogo zilizo sindikwa kunaweza  
kuchangia kupunguza upungufu wa bilioni 1.3 za kimarekani*



Kwa taarifa Zaidi:  
**Adebayo Abass, PhD**  
Mratibu, TAAT Cassava Compact  
Simu: +255 754 206 853  
Barua Pepe: a.abass@cgiar.org